

Sanaa Kwa Wote

KIMEHAMASISHWA NA KISA HALISI CHA MAISHA



Mwandishi: Olivia Wood

Mchoraji: Mariam Lasheen

Tafsiri: Mourice Wabwire



ASHOKA



Worldreader

“Sanaa Kwa Wote,” ni hadithi ambayo mwandishi amehamasishwa na kisa halisi cha maisha ya msichana mdogo kutoka Misri aliyegundua kuwa wakimbizi katika jamii yake walikuwa na ugumu wa kuzoea makaazi mapya. Alitaka kila mmoja kujihisi nyumbani na kuwa mwenye furaha! Akidhamiria kuchukua hatua, alitumia upendo wake wa sanaa kuwasaidia wakimbizi kujumuika katika jamii.

Hiki kitabu cha watoto cha picha ni tukio la ushirikiano baina ya Ashoka na Shirika la kibinafsi la Worldreader. Kimedhamiria kuwahamasisha watoto ulimwenguni kote kuwa wanamageuzi na kuwahimiza watu wazima kuwaunga mikono katika safari hizo.

Amira anaishi Alexandria na familia yake. Mji wa Alexandria upo nchini Misri- ni mji mkubwa wa kale katika Bahari ya Mediterenia. Misri ni nchi katika bara la Africa. Jua ni kali mno, bahari inang'aa kwa rangi ya samawati,na ina fukwe za mchanga.



Mjini, Amira anawaona wakimbizi wengi. Aghalabu wapo kando kando mwa barabara za mitaa na wanahitaji msaada. Shuleni, Amira anauliza swali kuhusu wakimbizi. Anajifunza kuwa wakimbizi ni watu ambao imewalazimu kutoroka nyumbani ili kupata ulinzi katika taifa jingine.



Mwalimu wa Amira anawaeleza kuwa, wakimbizi kutoroka vita, michafuko ama njaa kutoka nchi zao za kuzaliwa. Walikuja Misri wakitafuta pahali salama. "Misri ni nchi yenye upendo na ya kukaribisha watu. Familia kutoka sehemu za kijiografia tofauti na tamaduni mbalimbali huja Misri ili kuwa na maisha mazuri," Mwalimu wake aliliambia darasa.





Mwanafunzi mwenza tena rafiki wa Amira, Rama, ni mkimbizi kutoka nchi ya Syria. Siku moja baada ya shule Amira alimuuliza Rama kuhusu uzoefu wake kama mkimbizi.

Rama anamwambia jinsi anavyowapeza rafiki zake na mji wa nyumbani kwao. "Ilikuwa ni vigumu sana kuhama," Rama alisema, "bali familia yangu haikuwa na budi ila kuhamia mahali salama."

Rama alipenda sana kuimba na kusakata densi na rafiki zake nchini Syria. Amira anamsikiliza Rama akiongea kuhusu mila na tamaduni za familia yake.



Baada ya kujifunza kuhusu hadithi ya Rama, Amira alianza kugundua kuwepo kwa wakimbizi wengi katika maeneo yake. Nyumbani, alimuuliza mamake kuhusu maisha yao.

Mama yake alieleza, “Walishuhudia mambo mengi mabaya sana nyumbani kwao. Na si rahisi hivyo wanapokuja Misri. Huenda ikawa ni vigumu kupata ajira na nyumba. Wakati mwingine hawazungumzi lahaja ya kiarabu inayolingana na yetu jambo ambalo hufanya maisha yao kuwa ngumu hata zaidi.

Kwa sababu ya tofauti za lugha na tamaduni, wakimbizi huonewa na kuhisi kutokaribishwa. “Tayari wameshashuhudia wakati mgumu kama huo, tunafaa kuwaonyesha fadhili na upendo!” Aliambia mamake.

Amira anamuuliza mama yake kile ambacho wanawezafanya ili kuwasaidia wakimbizi katika maeneo yao. Wanachukua muda mrefu wakijadili jinsi ambavyo wanaweza kuwafanya wajihisi kukaribishwa nyumbani.

Mamake Amira anasema, “Na je, iwapo tungetumia sanaa yako kuwasaidia wakimbizi?”



Amira anapenda kuchora na kupaka rangi. Kuta zake nyumbani zimejaa michoro zenye rangi za kug'aa na maumbo tofauti tofauti. Kama vile rafikiye Rama, Amira anapenda aina zote za sanaa kama vile kuimba, densi na kuwasilisha jukwani. Sanaa humfanya Amira kuwa mwenye furaha, anapenda kuhadithia kuhusu kazi yake, familia yake na maisha yake.



Siku iliyofuata, Amira aliitembelea kambi ya wakimbizi. Alitaka kuandaa darasa la sanaa, na kuwakaribisha watoto wote wa maeneo hayo, kutoka kwa familia za wakimbizi na familia za Wamisri. Kambi ya wakimbizi inaungama kuwa hilo ni wazo zuri na Amira anapata rafiki zake wengi kumsaidia.



Siku ya kwanza ya somo lake, Amira alikuwa mwenye furaha. Kwenye kambi ya wakimbizi anacho chumba kilichojaa karatasi, rangi na penseli.

Pole pole, watu wanaanza kuwasili. Mwanzoni kila mmoja alikaa kimya. Amira alimkaribisha kila mmoja kujitambulisha na kutaja kitu cha kipekee kuhusu mji wake nyumbani. Rama alianza wa kwanza, alisakata densi ya kutoka utotoni mwake.

Mmoja baada ya mwengine walianza kufungua roho na kueleza kitu cha kipekee kujihusu. Baadaye walipaka rangi kwa pamoja.



Somo la sanaa lilofuata, darasa lilikuwa lenye uchangamfu sana. Kila mmoja alizungumza na mwenzake na kushiriki hadithi zao na tamaduni kupitia nyimbo, densi na ukumbi wa mawasilisho.

Amira anawatazama na kuwasikiliza. Anastaajabishwa na ueledi wao.

Baadhi ya familia zimevuka bahari na jangwa ili tu wafike Misri. Sasa hivi katika chumba kimoja hiki kila mmoja ana kitu maalum cha kushiriki.



Mwishoni mwa mwezi, Amira na rafiki zake wanaanda onyesho la sanaa. Kila mmoja anabandika mchoro wake kwa ukuta. Vijana wanasimama ili waimbe, wasakate densi, kuwasilisha skiti kwa rafiki zao pamoja na familia zao. Watu wa mjini walikuja kutazama mawasilisho yao.

Michoro ya rangi ni za kustaajabisha! Mawasilisho ni ya kipekee! Kuna hisia mingi sana kwa kila kipande cha sanaa hizo. Baadhi ni za huzuni na zingine ni za wingi furaha na matumaini.



Mwishoni mwa onyesho, baadhi ya familia zinamjia Amira. “Asante sana kwa kuandaa semina hii,” Wanasema. “Watoto wetu wameburudika katika kuhadithiana hadithi zao na kila mmoja. Wanajihisi wenye ujasiri na kukaribishwa katika jamii.”

Amira na rafiki zake wanajivunia mno. Tayari wanafikiria jinsi ambavyo watahusisha familia nyingine nyingi katika makaazi yao. “Ninaitarajia kwa hamu wakati ule kila mmoja atahisi kukaribishwa nyumbani Alexandria, na Misri kwa ujumla.



MATUKIO



ASHOKA



Worldreader

Tukio 1: Uangalifu

Kundi Umri: Umri Wote

Ujuzi: Huruma, Umahiri wa kudhibiti
Mihemko

Nyenzo: Karatasi, kalamu

Mbona?

Utafiti unadhihirisha kuwa kuna uwiano mkubwa baina ya uangalifu na uwezo wetu wa kuhurumisha. Uangalifu ni tukio la kuleta umakinifu wa kutambua hisia, mafikiria na mihemko ya kimwili. Uangalifu huandaa akili ya kisaikolojia kwa watoto na vijana na wavyohusiana, kuingiliana na kujifunza.

Jinsi

gani?

Hatua 1: Vuta hewa. Ili kuanza, hakikisha kila mmoja anafunga macho na uwaelekeze katika hatua zifuatazo. Toa kipande cha karatasi na kalamu. Kisha keti wima. Funga macho. Pumua ndani na nje kwa mara kadhaa. (Ingefaa zaidi ukitungia picha ama michoro: "Jaribu kuwazia kuwa kuna kamba inayovutwa juu ya vichwa vyenu.")

Hatua 2: Vuta pumzi | Baada ya kufanya mazoezi ya kupumua kwa nguvu kwa mara kadha, ni wakati wa kuvuta pumzi nzito. Fungua macho na uchukue kipande cha karatasi na kalamu.

Na kalamu katikati mwa karatasi pumua ndani na upumue nje tena, mara hii ukichora mstari kwa kila mpumuo. Usiinue kalamu kutoka kwa kipande cha karatasi. Unapopumua ndani, unachora mstari kwa upande wowote. Ukiendelea kuweka kalamu kwenye karatasi pumua nje na uchoe mstari. Endelea kufanya vivyo hivyo huku ukipumua ndani na nje, pole pole ukichora maumbo yako na kazi ya kiubunifu ya kisanaa.

Baada ya dakika moja au mbili, ongeza rangi katika kipande chako cha sanaa. Chora picha na miundo, kile kinachotokea kiasilia kwa kipande chako. Kipe kipande chako jina na umpe rafiki yako.

Tukio 2: Sahau kila kitu. Sasa tilia maanani kwa Mbona.

Kundi-umri: 3-12

Ujuzi: Huruma, Kufikiri kwa kina

Nyezo: Hamna

Mbona?

Hadithi hutufanya tuzame katika ulimwengu dhahania na kukumbana na wahusika, mazingira na matukio ambayo hawangeweza kukumbana nayo kwa hali hii ya kawaida. Kupitia hadithi tunajaza pengo la wahusika ambao maisha yao yana changamoto ambazo ni tofauti na zile zetu hivyo tunajifunza mambo mapya.

Tunapotazama na kusoma hadithi, aghalabu sisi hutilia maanani sana kwa kile kilichotokea ikilinganishwa na kwa nini kilitokea, kutalii fikira na hisia zilizochangia wahusika kujibu jinsi ambavyo walijibu. Badala yake, wacha tutalii fikira na hisia za Amira na Rama.

Vipi?

Chukua muda utafakari kile ulichosoma na kusikia, na jinsi ambavyo hadithi hizo zinavyowiana na maisha yenu ya kila siku.

Wacha tumzungumzie Rama:

- Je, unadhani ni vipi Rama anaweza kuwa akihisi kuhusu maisha yake mapya Misri?
- Je unajuaje?

Wacha tumzungumzie Amira:

- Je, nini kilichomfanya Amira kuongoza darasa la sanaa katika kambi ya wakimbizi?
- Je unafikiria Amira alihisi vipi wakati aliposimama kwa mara kwanza mbele ya watu waliokuwa wamekusanyika katika kongamano la Kisanaa?
- Mwishowe, darasa hili lilimfanya ahisi vipi?

Wacha tuzungumze kukuhusu

- Unaweza kufikia wakati ambapo ulihofia ama kuwa hatarini?
- Ni nini hukusaidia wakati ambapo unahisi kuhofia ama kuwa hatarini?
- Je ni lini ushawahi kuwa mjasiri? Ama ni lini ambapo ushawahi kumshawishi mtu mwengine kuwa mjasiri?

Tukio 3: Ndoto yako kwa Dunia

Kundi-umri: Miaka Yote

Ujuzi: Huruma, Ubunifu

Nyenzo: Vifaa vya kisanaa, karatasi; kalamu

Mbona?

Dunia yetu imejaa changamoto tele, uamuzi wa mtu mmoja unawezakuwa na athari kubwa katika jamii na tamaduni zake. Kuwa na matumaini ya maisha yajayo inatupa motisha tunayohitaji kuwa wanamageuzi. Huruma hutupa motisha kujenga kitu bora kwa pomaja na hutusaidia kupitia kwa mawazo dhahania na heshima- iliyoongozwa na kuelewa wa kina wa watu na mazingira yaliyotuzingira. Kwa kutazamia maisha bora yajayo hutupa motisha tunayohitaji kwa nguvu kama wanamageuzi.

Vipi? Toa kipande cha karatasi na nyenzo yoyote ya kisanaa uliyonayo. Wacha tufikirie kwa mapana kuhusu maisha yajayo. Chora dunia dhahania unayoitamia vile inavyofanana.

Unapochora, fikiria yafuatayo:

- Dunia inafananaaje pale ambapo kila mmoja, kwa mfano Rama anahisi kuwa nyumbani?
- Dunia inafananaje pale ambapo kila mmoja anachangia, kama vile vijana wa darasa la kisanaa?
- Dunia inafananaje pale ambapo kila mmoja anachangia, kama vile vijana wa darasa la kisanaa?
- Dunia inafananaje pale ambapo kila mmoja, kama Amira ni mashuhuri?
-

Bandika kipande cha mchoro wako nyumbani kama kikumbusho cha “dunia yako dhahania”. mwonyeshe kipande cha kisanaa mwanafamilia, rafiki au mwalimu. Waulize jinsi ambavyo dunia yao dhahania inavyofanana pia!

Meet Amira



Amira alipokuwa kijana, alipata mafunzo ya nyanjani na shirika la CARE International kuwasaidia wakimbizi kupata makazi mapya katika mji wake wa Alexandria, Misri. Wakati huo wa mafunzo ya nyanjani, alikutana na familia nyingi zilizoishi katika kambi za wakimbizi na alizungumza na kina mama na watoto kutoka nchi kama Sudani, Syria, Libya na Yemeni.

Aligemea shauku yake ya Sanaa na uchoraji kuzindua mradi wa kijamii, Ohana ili kuandaa makongamano ya Sanaa na tamaduni kwa vijana. Kwa malengo ya jamii ya wakimbizi yenye haki na umoja, Amira na rafiki zake wanatengeneza pahala salama pa watoto kujifunza kuhusu tamaduni tofauti na kujieleza kupitia densi, ukumbi wa Sanaa na michoro.

Leo hii, Amira amefuzu katika uwanja wa Sayansi ya maswala ya kisiasa. Anasema, “Ninataka kubadili kanuni za kitamaduni. Ili tubadili utamaduni, tunaweza kushiriki katika sanaa na mila baina ya wanajamii”.

Kuhusu Ashoka

Ashoka anaamini kuwa uwezo wa kuzoea na kuleta mabadiliko ni muhimu sana kwa kila mmoja kustawi haraka kwa huu ulimwengu unaobadilika. Ashoka anaandaa jamii ya kilimwengu yenye msingi ambapo kila mmoja ni mwanamageuzi. Katika nyoyo za kila mmoja Vuguvugu la Wanamabadiliko ni maono ya kubadilisha jinsi watoto na vijana wanakua na kupata ujuzi wa kuleta mabadiliko kwa mujibu wa wote.

www.ashoka.org

About Worldreader

Worldreader inaamini kuwa wasomi hujenga ulimwengu bora. Tunafanya kazi na washikadau ulimwengu mzima na kuwasaidia watu na jamii zilizopo katika mazingira dhaifu na usomi wa kidijitali ambao husaidia kuimasirisha kusoma na kuandika na matokeo ya kujifunza kwa watoto.

www.worldreader.org



Hakinakili © 2021 Ashoka and Worldreader

Hakinakili zimehifadhiwa. Kitabu hiki ama sehemu ya kitabu hairusiwi kuchapishwa ama kutumika kwa hali yeyote ile bila ya kibali kilichoandikwa na Ashoka ama Worldreader.

Kwa maswali zaidi tafadhali wasi liana nasi privacy@ashoka.org ama publishing@worldreader.org.